BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

MEI, 2025

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, Ambaye mikononi mwake umo Ufalme wote na yeye ni Muweza wa kila kitu, kwa kuweza kutujaalia uhai na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana hapa kwa lengo la kujadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yetu Tukufu kwa mwaka 2025/2026. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kutumia hekma, busara na weledi wa hali ya juu katika kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kudhihirisha uongozi makini unaofuata dira thabiti, wenye uimara wa maamuzi na dhamira ya kweli ya kuleta maendeleo endelevu katika kila sekta. Uongozi wake ambao umejikita katika kuimarisha misingi ya utawala bora, kukuza uwajibikaji na kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinatumika kwa ufanisi ili kuwanufaisha wananchi wote. Ni wazi kuwa kila mmoja wetu anaendelea kuiona Zanzibar ikipiga hatua kubwa katika sekta ya kiuchumi na kijamii kama ilivyo kipaumbele cha Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025.Kamati inamtakia kila la kheri Mheshimiwa Rais ili aweze kuchaguliwa tena kwa kishindo katika uchaguzi wa

2025/2030.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kwa umahiri wake na ujasiri unamfanya aweze kuiongoza Ofisi hii ambayo ina jukumu zito la kusimamia na kutekeleza miongozo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wa kupitia mswada huu wa makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya, kwa hakika wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa fedha zinazoidhinishwa zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | MakamuMwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Jamal Kassim Ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Abdallah Abass Wadi | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Ikulu ina jumla ya Programu kuu *saba (7)* ambazo ni fungu A01 Ofisi ya Rais Ikulu, fungu A02 Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, fungu A09 Taasisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini, na fungu A10 Taasisi ya Nyaraka na Kumbumbu Zanzibar. Kamati yangu kwa moyo mkunjufu kabisa imeridhika na utekelezaji wa programu zote zinazotekelezwa na Afisi hii ya Rais Ikulu kwa vile tulipata fursa ya kutembelea maeneo mengi, yaliyotuwezesha kupata taarifa njema za utekelezaji wa majukumu kupitia mafungu hayo. Tuna ziomba idara husika zenye kusimamia utekelezaji wake kuzidisha kasi ya maendeleo.

FUNGU *A 01* – AFISI YA RAIS IKULU

**Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Ikulu ambayo ndio muhimili mkuu wa uongozi, usimamizi, na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali wenye lengo la kuhakikisha maendeleo endelevu ya Zanzibar. kupitia utekelezaji wa programu kuu PA0101 ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha Mawasiliano Ikulu kwa dhamira ya kukuza utawala bora wa nchi yetu. Kamati inaipongeza Ofisi kwa kuonesha kwa vitendo, nia ya kuimarisha Mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu ya Zanzibar, Ikulu ya Dar es Salaam na Dodoma. Kwa kuwa, kamati ilitembelea na kuona kwa namna ambayo maboresho makubwa yalifanyika kwa mafanikio makubwa kupitia bajeti ya mwaka 2024/2025. Sambamba na hayo, kamati inaigiza wizara kuongeza kasi ya kufanya taratibu za ujenzi wa Ikulu ndogo ambayo inatarajiwa kujengwa Minyenyeni, Wilaya ya Wete, Pemba baada ya kukamilika kwa taratibu za awali na kupatikana eneo la ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati inaipongeza ofisi kupitia programu kuu ya Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu; kwa kuendelea kutangaza taarifa za Mheshimiwa Rais anapokuwa Zanzibar na nje ya Zanzibar kutokana na kazi zake kubwa na zenye kuleta tija kwa maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya SA010201 inayoratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, Kamati imeridhika na utekelezaji wake kwa kuwafikia na kuwapatia ushauri wana diaspora wote ambao wamesajiliwa kwa maslahi yao na maslahi ya uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu maendeleo ya diaspora na kuhakikisha wanakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo yetu kiuchumi na kijamii ili kwenda sambamba na fursa za kiuchumi na kijamii zinazopatikana katika Jumuiya za Kikanda na Kimatifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya SA010302 Uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti yenye lengo kuu la kuimarisha shughuli za mipango, kuandaa na kuchambua sera na kufanya tafiti. Katika utekelezaji wa programu hii, kamati inakiri kuridhishwa na utekelezwaji wa sheria mpya ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa **Namba 3 ya mwaka 2025.** ambayo tumeipitisha katika Baraza hili tukufu hivi karibuni.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kamati inaishauri wizara kufuatilia na kuhakikisha sheria hii inatekelezwa ipasavyo kwa kuwafikia wahusika wote na kuwapatia stahiki zao kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria. Kamati pia, inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kupitia programu hii kutoka bilioni 4.96 kwa mwaka 2024/25 na kufikia bilioni 9.07 kwa mwaka 2025/26 kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

## FUNGU *A 02* – BARAZA LA MAPINDUZI

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Afisi ya Baraza la Mapinduzi imepangiwa jumla ya TZS (Milioni Tatu, Laki Moja Elfu Saba na Senti Sita, Sifuri. Kati ya fedha hizo TZS (Milioni Moja, laki Moja Thamanini na Saba Elfu na Senti Tisa, Sifuri) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na TZS (Milioni Moja, Laki Tisa na Kumi na Tisa Elfu na Senti Saba, Sifuri) kwa ajili ya mshahara. Hadi kufikia Machi, 2025 Fungu A02 limeingiziwa TZS ( Milioni Mbili, Laki Moja na Thamanini Elfu na Senti Mbili, Tisa) Kati ya fedha hizo TZS. (Milioni Moja, Aroubaini na Saba Elfu na Senti Mbili, Sifuri) sawa na asilimia (Mia Moja na Nane Nukta Moja Nane) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na TZS. (Milioni Moja, Laki Moja , Thalathini na Tatu Elfu na Senti Sifuri Tisa) sawa na asilimia ( Sabiini na Nane Nukta Saba Sifuri) kwa ajili ya Mshahara.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa namna ilivyowapatia asilimia 108 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo hali iliwawezesha kusimamia majukumu yao ipasavyo na kuhakikisha Serikali yetu imara imefanikiwa katika usimamizi na utekelezaji wa maagizo yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Aidha, Kamati imeridhishwa na kazi kubwa inayotekelezwa kupitia programu kuu ya PA0202 ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kuwa na mfumo wa uendeshaji na utoaji wa huduma za kiofisi ulioimarika. Sambamba na kuimarisha mazingira ya kazi na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

### *FUNGU A 09* – TAASISI YA UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hii inatekeleza programu kuu mbili ambazo ni programu kuu ya PA0901 Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Serikali na Programu Kuu ya PA0902 Mipango ya Miradi ya Kipaumbele na Uendeshaji. Taasisi hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufuatilia miradi ya vipaumbele katika sekta za uchumi wa buluu, elimu, afya, maji uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kilimo. Kamati inaunga mkono juhudi hizo na kuishauri ofisi kuzidisha bidii katika kufuatilia na kusimamia miradi ya maji safi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia, inaishauri taasisi hii kuendelea kuimarisha uwezo wa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ambayo yatakaongeza ufanisi wa kazi zao katika kufuatilia na kusimamia miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa kasi zaidi kwenye awamu hii ya nane. Ni matumaini yetu kuwa ufuatiliaji na usimamizi bora utasaidia kupata miradi yenye ufanisi na kukuza maendeleo ya nchi yetu.

### *FUNGU A10* – TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Nyaraka na Kumbumbu inatekeleza programu ya msingi ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu kwa matumizi ya Serikali na ummakupitia fungu PA1001. Kamati ilipata fursa ya kuutembelea mradi unaotekelezwa wa ujenzi wa jengo jipya la ghorofa tano lenye lengo la kuondoa changamoto ya ofisi kwa watendaji na kuweka maendeo muhimu ambazo yanahitajika kwa ajili ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za taifa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na uamuzi huu wa ujenzi wa jengo jipya la kisasa ambalo litakapokamilika litaimarisha uhifadhi wa urithi wa kihistoria na kuchangia ukuaji wa uchumi kupitia uhamasishaji wa tafiti, utalii na huduma mbalimbali kama kitovu cha historia na tamaduni za Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali baada ya kukamilika kwa ujenzi huu unaoendelea kuandaa mradi maalumu kwa ajili ya fedha za kununulia vifaa vya kisasa vya kulinda na kuhifadhi nyaraka kwa maslahi ya taifa na vizazi vijavyo.

### *HITIMISHO*

**Mheshimiwa Spika,** haitokuwa busara kama sitomalizia hotuba hii kwa kumshukuru Rais wetu mpendwa Mheshimiwa, Dkt. Husein Ali Mwinyi kwa namna anavyoisimamia Serikali kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati, miradi ya kiuchumi na kijamii ambayo imempa umaarufu mkubwa kwa wananchi na mataifa yanayoizunguka

Zanzibar.

Ushauri wetu ni kuwaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuisimamia kikamilifu miradi hii na kuhakikisha tunaiunga mkono katika utekelezaji wake kwa lengo la kutimiza azma ya Serikali yetu kwa kuwatumikia wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, nihitimishe kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waichangie, wairidhie Bajeti hii na hatimae waiidhinishie Ofisi ya Rais Ikulu, Makadirio ya Mapato na Matumizi Fedha zilizopangwa ili wapate kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………….……………..

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

<u>ZANZIBAR</u>